**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Halmashauri ya Manispaa ya Temeke**

**Shule ya Sekondari Mikwambe**

**S.L.P 36014**

**16/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MIKWAMBE HALMASHAURI YA TEMEKE MKOA DAR ES SALAAM MWAKA 2024/25**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/25 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Mikwambe ni shule ya mchanganyiko ya kutwa, yenye kidato cha kwanza mpaka sita. Kwa kidato cha tano na sita wanafunzi wanasoma Tahasusi za HGL, HGK, HKL na HGLi. Shule ipo umbali wa Kilometa 13 toka Kigamboni  na Kilometa 10 toka Mbagala Usafiri wa daladala unapatikana katika vituo vya Kigamboni (mabasi ya Kigamboni - Mbagala/Mwandege) au kituo cha Mbagala Zakheim (mabasi ya Mbagala - Kigamboni) unashuka kituo cha Mikwambe.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024 akiwa ameambatana na mzazi/mlezi wake. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 08/07/2024

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

#### 2.1.1 Wasichana

i. Sketi mbili (2) ndefu za bluu (aqua blue), mshono rinda-box. Shati (2) nyeupe (pamba) mikono mirefu.
ii. Nguo itakayovaliwa ndani ya shati iwe nyeupe mfano fulana (singlet).
iii. Viatu vya ngozi vyeusi (jozi mbili) viwe vya mkanda kati, vinafunika kabisa (visiwe vya wazi) na visiwe na kisigino kirefu wala urembo.
iv. Soksi nyeupe ndefu (Stocking) sio za kuonyesha mwili (transparent), jozi mbili.
v. Sweta bluu.
vi. Watakaovaa Hijabu (iwe ndefu mpaka kwenye vifundo vya mikono) watatumia nusu kanzu badala ya shati.
vii. T-shirt nyuesi ya kola inapatikana shuleni kwa shilling elfu kumi na tano.
viii. Wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele za mistari ya kurudi nyuma (twende kilioni) zisipungue tano na zisizidi saba, kwa wasiosuka wanapaswa kuwa na nywele fupi
ix. Nembo ya Shule (inapatikana shuleni.

#### 2.1.2 Wavulana

**i.** Suruali mbili (2) rangi ya bluu (aqua blue) isiwe modal **(iwe kati inchi 15 na 18)**
ii. Shati nyeupe mbili (2) mikono mirefu (pamba).
iii. Nguo itakayovaliwa ndani ya shati iwe nyeupe mfano fulana (singlet).
iv. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba, jozi mbili (2), (shingo fupi).
v. Soksi nyeusi jozi 2.
vi. T-shirt nyuesi ya kola inapatikana shuleni kwa shilingi elfu kumi na tano.
vii. Mkanda mweusi wenye bakoli ya kawaida.
viii. Sweta bluu.
ix. Nembo ya shule (inapatikana shuleni).

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari (counter books) angalau saba;

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Scientific Calculator (HGL,HGLi na HGK);
v. Mathematical set (HGL, HGLi na HGK)
vi. Vifaa vya usafi.
   a) HGK – Jembe na brashi ya choo
   b) HGL – Jembe na fagio la ndani (soft broom)
   c) HKL – Kwanja na dawa ya chooni
   d) HGLi – Fagio la ndani (soft broom) na ufagio wa nje (chelewa)

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

Fedha zote za michango zilipwe kupitia akaunti ya shule yenye Namba ***A/C*** **20101100236 NMB**. Jina la Akaunti ni **MIKWAMBE SECONDARY SCHOOL**. Baada ya nakala ya malipo ya benki (**BPS)** yenye jina la mwanafunzi ziwasilishwe shuleni.

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha mbili (2) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**……………………………………..**

**JANATH R. MZEE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa Shule 0784 424 258**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0717 434 816**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0756 969 542**
- **Mwalimu wa Malezi 0713816 732**